{«DateLetterGenerated»}

Mkazi Mpendwa,

Mahali unapoishi katika {«Street, City, State Zip»} palipatikana kuwa na viwango visivyo salama vya madini ya risasi ambavyo vilichangia sumu ya madini ya risasi kwa mtoto. Mfiduo wa madini ya risasi unaweza kuharibu ubongo na mfumo wa neva, kuchelewesha ukuaji na maendeleo na kusababisha matatizo ya kujifunza na tabia pamoja na matatizo ya kusikia na kuzungumza.

Sababu ya kawaida zaidi inayowafanya watoto waathiriwe na sumu ya madini ya risasi ni rangi ya madini ya risasi iliyoharibika (vumbi) katika nyumba za zamani zilizojengwa kabla ya 1978. Vyanzo vingine vinavyowezekana vya mfiduo wa madini ya risasi ni pamoja na udongo, maji na bidhaa za watumiaji.

Ikiwa mtoto mwenye umri wa chini ya miaka 6 anaishi nyumbani kwako au anakaa huko kwa zaidi ya saa sita kwa wiki, Idara ya Afya ya Ohio inapendekeza kwamba mtoto huyo afanyiwe kipimo cha damu na daktari au mtoa huduma mwingine wa afya ili kuhakikisha kwamba hajaathiriwa na sumu ya madini ya risasi.

Shirika la {«HDname»} lilimwamuru mmiliki wa nyumba unakoishi kama mmiliki wa jengo arekebishe matatizo ya madini ya risasi lakini anakataa kufanya hivyo. **Kutokana na hali hiyo, sheria ya Ohio inasema kwamba mtu yeyote anayeishi katika nyumba hio lazima ahame kwa sababu imetangazwa kuwa si salama kwa watu kuishi hapo. Ni hatari hasa kwa watoto wenye umri wa chini ya miaka 6 na wanawake wajawazito.** Ishara ya onyo iliwekwa kwenye jengo na ni kinyume cha sheria kuiondoa. ODH hufuatilia majengo kama hayo ili kuhakikisha kwamba ishara za onyo bado zipo na kwamba hakuna mtu anayeishi humo.

Unahitaji kutafuta nyumba tofauti ya kuishi (jengo lililojengwa baada ya 1978 ikiwezekana, kwani kuna uwezekano mdogo kwamba litakuwa na matatizo ya madini ya risasi, pia). Jamii nyingi za Ohio zina mashirika ya huduma za jamii au rasilimali nyingine za jamii ambazo zinaweza kukusaidia kupata mahali pengine pa kuishi. Unaweza kuona orodha ya majengo ya kuepuka katika eneo lako kwa sababu pia yana matatizo ya madini ya risasi (inapatikana kwenye tovuti ya ODH katika http://www.odh.ohio.gov/pbhazproperties).

Ikiwa una maswali kuhusu taarifa hii au kuhusu jinsi ya kuhakikisha mtoto anapimwa sumu ya madini ya risasi, piga simu kwa {«HDname»} kupitia {«HDPhone»}.

Kwa Uaminifu,

{«HDRepresentativeName»}
{«HDRepresentativeTitle»}
{«HDName»}